Jarida la Shirika la Uboreshaji Mifereji ya Asili na Uhifadhi wa Mazingira (TIP)

# Maendeleo ya TIP

Toleo la 5 Februari 2004



## "Safisha mfereji upate maji mengi"

*"Na Jan Moejes"*

Kwa miaka mingi iliyopita shirika la TIP limejulikana sana Tanzania. Mifumo ya umwagiliaji ya asili ambayo TIP imeisaidia na kuiboresha, imekuwa ikitembelewa na wageni wengi kila mwaka. Wengi wa wageni hao ni wakulima kutoka sehemu nyengine za Tanzania na pia kutoka nchi za Africa Mashariki (Kenya na Uganda). Na wageni muhimu sana ni wafadhili wanaoiwezesha TIP kusadia wakulima wadogo wadogo katika kilimo cha umwagiliaji kutumia mifereji ya asili.

Kuna usemi wa Kichina unasema "**picha husema mengi kuliko maneno mengi**" ikiwa na maana kwamba kuona kunavutia na kuelimisha zaidi kuliko kusoma maneno peke yake. Na hii huweka kumbukumbu nzuri kwa wageni endapo wataona kitu cha kujifunza kwenye mfumo wako wa umwagiliaji na kile watakachosikia kutoka kwako. Kile watakachoona ni kitu gani? Je matuta yako sawa na imara? Je mashamba ni masafi au yamejaa majani? Je mifereji imefanyiwa usafi au kingo zake zimebomoka na umefunikwa na uoto wa majani?




Utunzaji mzuri wa mfumo wa umwagiliaji hutoa mvuto kwa wageni kuutembelea. Utunzaji huonyesha uimara wa mfumo na ushirikiano uliojengeka, maamuzi ya pamoja na umilikaji wa wakulima. Mfano; Wafanyabiashara wakubwa wa nje wanapenda kushirikiana kibiashara na wakulima ambao mashamba yao ni masafi yanayotunzwa vizuri kwa sababu inaonyesha ni jinsi gani mkulima alivyo makini katika uzalishaji na kupanda mazao yaliyo bora. Kingo fupi na nyembamba za mifereji pamoja na mashaba ambayo hayajahifadhiwa vizuri husababisha upotevu wa maji.

Kunahitajika kufanyika usafi wa mara kwa mara na ukarabati wa mifereji ili kuzuia upotevu wa maji ya umwagiliaji. Mwendo kasi wa maji unaotakiwa katika mfereji hupungua endapo mfereji utaachwa na maotea ya majani.
Nini kinahitajika katika utunzaji bora wa mfumo?

**Cha kwanza** ni muda na nguvu kazi. Matengenezo ya kila mara yatasaidia mfumo kuwa katika mahali pazuri na itapunguza wingi wa kazi. Inashauriwa kuufanyia usafi mfumo wa umwagiliaji angalau mara moja kwa wiki.

**Cha pili** pesa huhitajika katika kukarabati sehemu za mfereji. Ni vyema Kikundi cha Watumia Maji (WUG) kikawa na akiba benki. Ada wanazotoa wakulima ziwekwe benki mpaka wakati matengenezo yanapohitajika.

**Cha tatu** muhimu ni mfumo mzuri wa umilikaji wa mfereji. Kikundi kinatakiwa kuwa na sheria ndogo ndogo za matengenezo pamoja na ada ya matengenezo. Kamati inayoshungulika na mfumo mzima wa umwagiliaji inayo jukumu la kukagua utunzaji wa mfereji. Kamati ina uwezo wa kuwatoza faini wakulima ambao hawakutunza maeneo yao ya mfumo wa umwagiliaji kwa sababu utunzaji mbaya sehemu moja ya mfumo wa umwagiliaji huathiri upande mwingine wa mfumo.

Hivyo mfumo wa umwagiliaji unaotunzwa vizuri, utawavutia wageni kuwatembelea, utakufanya ujivunie, mbali na yote hayo utakuzalishia zaidi kwa sababu "Safisha mfereji upate maji mengi"

### YALIYOMO

Ujasirishaji wa wazalishaji na kuwaunganisha ..... 2
Shukurani... 2
Uhifadhi wa ardhi katika maeneo ya kilimo....... 3
Usafirishaji wa maji ya Umwagiliaji kwa........... 4

*TIP ni shirika lilosajiliwa chini ya sheria ya mashirika (Cap. 375) tarehe 6 Agosti 1999*

# Ujasirishaji wa wazalishaji na kuwaunganisha na masoko: Arumeru

*"Na Loyce Kaitira*

Shirika la uboreshaji wa mifaereji ya asili na uhifadhi wa mazingira (TIP) limekuwa moja ya taasisi shiriki katika kuwezesha utekelezaji wa Mpango wa Kuendeleza Mifumo ya Masoko ya mazao ya Kilimo (AMSDP) katika wilaya ya Arumeru, Mkoani Arusha. Mpango huu umebuniwa ili kuwashirikisha kwa ukamilifu wakulima wadogowadogo na wafanyabiashara ndogondogo katika masoko na kuwaongezea tija kutokana na mazao ya kilimo pamoja na shughuli nyingine zinazohusiana na masoko. Malengo mahususi ya mpango huu ni:

(i) Kuwawezesha wakulima wadogo wadogo kuongeza uzalishaji wa mazao mbalimbali an kushiriki katika mfumo wa masoko ulioboreshwa.

(ii) Kuwezesha upatikanaji wa vitendea kazi kwa wafanyabiashara ndogondogo wanaokaa katika maeneo ya vijijini na kuwaunganisha na wakulima wadogo wadogo.

Kwa kushirikiana na wafanyakazi wa Halmashauri ya wilaya ya Arumeru, TIP itawezesha utekelezaji wa kipengele cha pili cha mpango huu kabambe kijulikanacho kama Ujasirishaji wa wazalishaji na kuwaunganisha na masoko.. Uwezeshaji wa wakulima wadogowadogo na wafanyabiashara ndogondogo ndani ya mpango huu, utakuwa ni kwa njia ya vikundi. Walengwa watalazimika kuunda vikundi kwanza. Vikundi hivyo vitaimarishwa kabla ya kuanza rasmi kwa shughuli za masoko. Shughuli zote za mpango huu zitafanyika katika maeneo maalumu yatakayochaguliwa kwa ajiri ya utekelezaji ndani ya wilaya.

Kwa kipindi cha mwezi Januari hadi Juni 2004, TIP itafanya shughuli zifuatazo:

(i) Kubainisha vikundi vilivyopo na kuunda vikundi vingine vipya kwa wakulima wodogo wadogo

Kazi hii itafanyika kwenye maeneo yaliyoainishwa kwa kutumia taarifa mbalimbali zilizopo na pia mikutano ya kuhamasisha. Vikundi vitkavyochaguliwa vitafanyiwa upembuzi yakinifu ili kujua matatizo na mikakati waliyonayo katika kutatua matatizo yanayowakabiri.

(ii) Mpango wa utekelezaji kwa kila kikundi

Vikundi vitwezeshwa kuandaa mpango kaziambao utatumika kama mwongozo katika kuandaa mapendekezo ya utekelezaji wa mradi ndani ya vikundi. Mapendekezo hayo yataeleza bayana matatizo na mikakati ya vikundi katika kutatua matatizo yao. Pia mipango na mikakati ya siku za usoni.

(iii) Kuandaa mafunzo ya kuimarisha vikundi

Mitaala iliyopo itaboreshwa ili kukidhi mahitaji ya mafunzo ya vikundi husika. Uandaaji wa vitini na ratiba ya mafunzo kwa kila kikundi utafanyika katika hatua hii. Kazi hii itafanywa kwa ushirikiano na wadau wengine ili kuwezesha utekelezaji shirikishi wa mpango huu.

(iv) Kubainisha/kuunda vikundi vya wanyabiashara ndogo ndogo

Kufuatia mikutano ya uhamasishaji, vikundi vya wanyabiashara ndogondogo vitaundwa. Vikundi vitakavyochaguliwa vitasaidiwa kulingana na mahitaji yao. Vikundi hivyo vitapata mafunzo ya biashara na pia kufanya utafiti wa masoko au wateja. Vikundi vitaunganishwa na wakulima wadogo wadogo ili kuwezesha upatikanaji wa masoko ya uhakika.

Na tuutakie kheri na mafanikio mema mpango huu kabambe huko Arumeru!!



**Barua za wasomaji**

Tunakaribisha maoni, mapendekezo, hadithi, na fikra yoyote yenye kuelimisha jamii ili tuchapishe.Tuandikie ukionyesha jina kamili na anwani kwa:
TIP, Box 8909 Moshi,Kilimanjaro

**Shukrani!!!**
Shukrani za pekee ziwaendee
NOVIB, UBALOZI WA JAPANI, UBALOZI WA UHOLANZI na SHIRIKA LA MAENDELEO LA UMOJA WA MATAIFA (UNDP)
Kwa ufadhili wa shughuli za TIP

# UHIFADHI WA ARHI KATIKA MAENEO YA KILIMO CHA UMWAGILIAJI CHINI YA UANGALIZI WA TIP

*"na Peter Mjata"*

Uhifadhi wa udongo na maji pamoja na upandaji wa miti huwezesha unyevu nyevu katika udongo kukaa kwa muda mrefu kwa ajili ya mimea na viumbe wengine waishio ndani ya udongo. Hii huimarisha matumizi mazuri ya maji wakati wa umwagiliaji na kusaidia kuongezeka kwa uzalishaji.

Kwa kutumia njia ya ushirikishwaji, wataalamu wa TIP pamoja na wakulima huchanganua na kujadiliana kuhusu mbinu za kuhifadhi ardhi ambazo kwao wamezoea kuzitumia, vifaa asilia watumiavyo na utaalamu wa asili waujuao na watumiao katika kuhifadhi maeneo ya umwagiliaji. Zoezi hili hufanyika kabla ya uhifadhi wa udongo na maji na upandaji wa miti (SWC & Af-forestation). Pia hupima udongo na mwinuko wa mashamba yao. Hii huwawezesha kujua ni njia ipi inayofaa kutumika ili kuweza kuhifadhi ardhi ambayo haijahifadhiwa vizuri katika maeneo ya umwagiliaji.

Baada ya uchanganuzi na majadiliano, shirika la TIP huandaa mafunzo kwa ajili ya kupata wataalamu wenza (VTs) yanayohusu utaalamu wa kilimo pamoja na uhifadhi wa udongo kwa njia ya matuta na njia ya upandaji wa mimea. Ndani ya mafunzo kunakuwepo na ziara na mafunzo pamoja na kutengeneza vishamba vya maonyesho. Ziara za mafunzo pamoja na vishamba vya maonyesho huwapa nafasi wakulima kutumia au kuboresha mbinu zao walizozizoea kutumia katika kuhifadhi ardhi kwa njia madhubuti na ya kuwezesha kukua kwa uchumi wao.

Matokeo yanayotarajiwa kutokea baada ya mafunzo ni kuzuia mmomonyoko wa udongo unaosababishwa na maji ya umwagiaji, kuhifadhi udongo katika maeneo ya umwagiliaji, kuhifadhi unyevu nyevu wa udongo, uangalizi mzuri wa miundombinu ya umwagiliaji pamoja na kuhakikisha kuwa mfumo wote wa asili wa umwagiliaji unaboreka.



*Wakulima wa Kikundi cha Watumia Maji cha Heigugu Wilayani Mwanga wakiendesha kitalu cha miti baada ya kupata mafunzo ya uhifadhi wa udongo na maji*

**EPUKA UKIMWI UKUZE UCHUMI WAKO**

**UKIMWI husababisha vifo na kupungua kwa nguvu kazi ambazo ni tegemeo la nchi yetu kukuza uchumi wake.**

**NDUGU EPUKA UKIMWI NI HATARI KWA MAISHA YAKO**

Shirika la Uboreshaji Kilimo cha Umwagiliaji wa Mifereji Asili na Mazingira ni shirika lisilo la kiserikali lililosajiliwa tangu 1999. Hata hivyo shirika hili lisilo la kiserikali lililoundwa mnamo mwaka 1988, wakati ambao TIP lilianzishwa kama Mpango wa Uboreshaji Mifereji ya Asili chini ya waasisi wa shirika la Maendeleo la Uholanzi (Netherlands SNV).
TIP inashirikiana na Halmashauri za Wilaya ili kuweza kuwafikia kwa urahisi walengwa ambao ni wakulima wa maeneo ya umwagiliaji kwa mifereji ya asili. Malengo ya TIP ni kuboresha na kuinua viwango vya maisha ya jamii za maeneo ya Tanzania yenye ardhiinayofaa kwa kilimo cha umwagiliaji kwa kutumia mifereji ya asili kuhifadhi maji na udongo, kustawisha misitu na maeneo yavyanzo vya maji nchini Tanzania.

**TIP NI MSAADA WAKO WA MAENDELEO**

Malengo makuu mnne:
- Usimamizi madhubuti na uhusiano wa kijinsia
- Kuhifadhi ardhi na maji
- Kuboresha mifereji ya asili
- Wakulima na Masoko

*Wasiliana nasi Katika ofisi zetu Moshi*




Kwa maelezo zaidi tafadhali Wasiliana nasi katika Ofisi yetu ya Moshi

S.L.P 8909, Moshi - Kilimanjaro
SIMU: 027 53025/54232
FAX: 027 51124
E-Mail: tip@eoltz.com
Website: www.tiptz.org

## Usafirishaji wa maji ya Umwagiliaji kwa kutumia Mabomba

*"Na Eng. A.L. Maro"*

TIP imeamua kuuendeleza na kuuboresha utaalamu wa kutumia bomba badala ya mfumo wa mifereji kwa sababu zifuatazo:-

a) kupunguza upotevu wa maji wakati wa kusafirisha
b) kuongeza ufanisi wa umwagiliaji
c) ni mfumo wa umwagiliaji ambao hausababishi mmomonyoko wa udongo

Kwa mfumo wa umwagiliaji ambao haujasakafiwa wenye uwezo wa kusafirisha maji kwa kiasi cha lita 5 – 20 kwa sekunde, ni gharama nafuu kutumia mfumo huu wa mabomba kutokana na upotevu mwingi wa maji ambao huweza kutokea ukitumia mfereji. Pamoja na hayo, maeneo mengi ambayo TIP hufanya kazi ni maeneo ya milima, usanifu unahakikisha kwamba maeneo yote yanapata maji ya umwagiliaji kuanzia banio (intake) mpaka kwenye mashamba ya umwagiliaji

Gharama ya mfereji uliosakafiwa kwa urefu wa mita moja wenye uwezo wa kusafirisha maji lita 20 kwa sekunde ni Tsh. 18,000/=. Lakini mabomba yajulikanayo kama PVC kiwango "B" hupunguza gharama kufikia kiasi cha sh. 7,000/=. Mfumo huu mpya umejaribiwa na kuonyesha mafanikio katika Eneo Bonde la Chome wilaya ya Same na Mlombola wilaya ya Mwanga.

Wakulima huchangia gharama za kuchimbia mabomba pamoja na kujijengea visima vidogo kwa kila mkulima.

Matokeo;
a) Imeongeza eneo la umwagiliaji kwa ekari 14 Wilaya ya Mwanga na ekari 5 katika wilaya ya Same baada ya kutumia mfumo huu wa kusafirisha maji ya umwagiliaji kwa kutumia mabomba.
b) Uzalishaji kwa kila eneo umeongezeka kwa asilimia 20%
c) Kumeongezeka ufanisi wa umwagiliaji kutoka asilimia 30% mpaka asilimia 65%




MFUMO WA KUSAFIRISHA MAJI YA UMWAGILIAJI KWA KUTUMIA MABOMBA